

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



**YAH: TANGAZO LA KAZI AJIRA YA MUDA**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (Land Tenure Improvement Project). Hivyo katika utekelezaji huo inawatangazia Wakazi wote Wilaya ya Dodoma kuomba nafasi za kazi za Vibarua, katika nafasi zifuatazo

**NAFASI:** Wakusanya Taarifa za Vipande vya Ardhi (Land Data Collectors)

**IDADI:** WATU 18

**AINA YA AJIRA:** Siku 21 za Kazi

**A. Sifa za waombaji:**

- Awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18
- Awe na elimu/ujuzi wa angalau Stashahada katika fani zinazohusiana na ardhi kutoka katika Chuo chochote kinachotambulika na Serikali
- Aweze kutumia vifaa vya kisasa (mobile devices) kukusanya taarifa za wamiliki ardhi
- Uwezo wa kutumia mifumo ya kijiografia (GIS)
- Waliowahi kutumia simu janja kukusanya taarifa za ardhi watapewa kipaumbele

**MAJUKUMU**

1. Kukusanya taarifa za vipande vya ardhi katika maeneo ya urasimishaji.
2. Kuchukua taarifa za matumizi ya ardhi

3. Kuchukua taarifa za umiliki wa vipande vya ardhi.
4. Kuchakata taarifa zilizokusanywa.
5. Kushirikiana na kamati za urasimishaji katiaka kuwafikia wananchi ili kuchukua taarifa za vipande vya ardhi.
6. Kutunza vifaa vya ukusanyaji taarifa.
7. Kutekeleza majukumu mengine kadili ya maelekezo ya viongozi wa mradi.

#### **B. Namna ya Kuwasilisha Maombi ya kazi.**

Mwombaji awasilishe maombi kwa mkono katika Ofisi za Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi zilizopo katika Jengo la Kambarage – Dodoma (ghorofa ya kwanza mkabala na CRDB Benki) kwa anuani ifuatayo;

Mratibu wa Mradi,  
Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi,  
S. L. P 2908,  
**DODOMA.**

#### **Viambatanisho**

1. Barua ya Maombi
2. Wasifu (CV)
3. Cheti cha elimu inayoendana na masula ya Ardhi

*Maombi yawasilishwe kuanzia Tarehe 09.03.2023 saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 11 Machi, 2023 saa 06:30 mchana.*

*Limetolewa na Mratibu wa Mradi*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



**YAH: TANGAZO LA KAZI AJIRA YA MUDA**

**NAFASI:** WAADIZI WA UPIMAJI (FIELD ASSISTANTS)

**IDADI:** WATU 24

**AINA YA AJIRA:** Ajira ya Siku 21 zinazoweza kuongezwa

**Sifa za waombaji:**

- Awe Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea
- Awe anajua kusoma na kuandika
- Mwenye uzoefu wa kusaidia wampima ardhi katika usimikaji wa vigingi atapewa kipaumbele

**MAJUKUMU**

1. Kusaidia katika kubeba vifaa vya upimaji katika maeneo ya urasimishaji.
2. Kuwasaidia wapima katika kuweka alama za mipaka ( Becons ).
3. Kutekeleza majukumu mengine kadili ya maelekezo ya viongozi wa mradi.

**C. Namna ya Kuwasilisha Maombi ya kazi.**

Mwombaji awasilishe maombi kwa mkono katika Ofisi za Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi zilizopo katika Jengo la Kambarage – Dodoma (ghorofa ya kwanza mkabala na CRDB Benki) kwa anuani ifuatayo;

Mratibu wa Mradi,  
Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi,  
S. L. P 2908,  
**DODOMA.**

### **Viambatanisho**

1. Barua ya Maombi iliyoandikwa kwa Mkono

*Maombi yawasilishwe kuanzia Tarehe 09.03.2023 saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 11 Machi, 2023 saa 06:30 mchana.*

*Limetolewa na Mratibu wa Mradi*